ORODHA YA NYARAKA NA TAARIFA ZA MAOMBI YA LESENI YA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA DARAJA LA 2 (TIER 2) - ZANZIBAR

Jina la Mwombaji (Taasisi): …….

Tarehe ya kuwasilisha maombi: …….

Tafadhali jaza **NDIO** kwa taarifa zilizo wasilishwa, **HAPANA** kwa taarifa ambazo hazijawasilishwa na **HAIHUSIKI** kwa taarifa zisizotakiwa kwenye maombi yako.

Rejea *Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar (Watoa Huduma Ndogo za Fedha wasiopokea Amana), 2025*.

Maelezo ya Jumla kwa Mwombaji

1. Mwombaji lazima awe amesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Nam.15 ya 2013 au sheria nyengine yoyote husika au jina la kibiashara la mmiliki binafsi.
2. Jina la kibiashara la mwombaji lazima liwe na maneno yafuatayo “microfinance”, “finance”, “financial Services”, “financial solution”, “credit” au “microcredit.”
3. Mwombaji anatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi isiyorudishwa ya kiasi cha shilingi 500,000:

   Akaunti Na: 9944713001
   Jina la Akaunti: MFCs & FICOs Applicant Fees
   Maelezo ya Uhamisho wa Fedha: Ada ya Malipo ya (Weka Jina la Mwombaji)

4. Maombi ya Leseni ya kufanya biashara ya Huduma Ndogo za Fedha Daraja la Pili (Tier 2) Zanzibar yanaweza kuwasilishwa Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania (Dodoma) au katika ofisi za matawi yake yaliyopo Mwanza, Dodoma, Mbeya, Mtwara, na Arusha, na ofisi za Makao Makuu-Ndogo zilizopo Dar es Salaam na Zanzibar.

ZINGATIA : Benki Kuu ya Tanzania itapokea na kuyachakata maombi yaliyokamilika pekee, yenye nyaraka zilizoorodheshwa hapa chini.

Orodha ya Nyaraka Zinazohitajika kwa Ajili ya Maombi ya Leseni ya Kufanya Biashara ya Huduma Ndogo za Fedha Daraja la Pili (Tier 2)

Na.	Jina la Nyaraka	Nyaraka Imeambatanishwa
	Mwombaji anatakiwa kuweka jibu (Ndio, Hapana, Haihusiki)	
	A. Kwa waombaji wote	
1.	Barua ya maombi kama ilivyoainishwa chini ya jadweli la kwanza la *Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar (Watoa Huduma Ndogo za Fedha wasiopokea Amana), 2025*	
2.	Swifti ya benki au nyaraka nyengine yoyote inayokubalika na Benki inayothibitisha malipo ya ada	
3.	Uthibitisho wa chanzo cha mtaji kwa wamiliki au wanahisa wa kigeni (mfano Taarifa za fedha zilizokaguliwa za kampuni zinazomilikiwa na mwombaji, hati ya mshahara, cheti cha malipo ya gawio la hisa inayoonesha idadi ya hisa zinazomilikiwa na gawio lililolipwa, kodi ya	

Na.	Jina la Nyaraka	Nyaraka Imeambatanishwa
	Mwombaji anatakiwa kuweka jibu (Ndio, Hapana, Haihusiki)	
	nyumba - ambatanisha hati ya umiliki wa nyumba/mali, hati za malipo ya riba kutoka kwenye hati fungani au nyaraka za madeni au uthibitisho mwingine unao fanana na vithibitisho hivyo tajwa).	
4.	Uthibitisho wa uwepo wa mtaji (taarifa ya akaunti ya benki inayoonesha kiasi kisichopungua shilingi 50,000,000 kwa Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha anayemilikiwa na wazawa, na shilingi 100,000,000 kwa Mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha anayemilikiwa na wageni).	
5.	Nakala zilizothibitishwa za vyeti vya taaluma na utaalam kwa kila mmiliki, mjumbe wa bodi ya Usimamizi na afisa mtendaji mkuu.	
6.	Sera ya Mikopo inayozingatia mambo ya msingi yaliyoainishwa kwenye Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar (Muundo wa sera ya ukopeshaji unapaswa kuzingatia Kanuni ya 36), kama ifuatavyo;	
	(a) taratibu za ukopeshaji na nyaraka zinazohitajika;	
	(b) masharti ya kupata mkopo;	
	(c) aina za mikopo, muda na awamu za ulipaji;	
	(d) aina za dhamana zinazokubalika;	
	(e) ukomo wa mkopo kwa mkopaji na bidhaa za mkopo;	
	(f) gharama za mkopo ikiwemo viwango vya riba, ada na tozo; (Riba inatakiwa kukokotolewa kwenye kiasi cha mkopo halisi kilichosalia 'reducing balance')	
	(g) utaratibu wa kuidhinisha mkopo;	
	(h) tathmini ya uwezo wa mkopaji kurejesha mkopo;	
	(i) masharti ya udhamini wa mkopo, kama yapo;	
	(j) ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa mikopo;	
	(k) kipindi kinachotolewa kabla ya kuanza kurudisha mkopo, kama kipo;	
	(l) utaratibu wa ukusanyaji na ufuatiliaji wa mikopo;	
	(m) vigezo na taratibu za kurekebisha masharti ya mikopo;	
	(n) muda unaotumika kushughulikia mkopo baada ya kupokea maombi ya mkopo yaliyokamilika; na	
	(o) vigezo na taratibu za kuidhinisha na kuruhusu zinazotakiwa kwa ajili ya kufuta mikopo isiyolipika	
7.	Fomu ya maombi ya mkopo ioneshe kiwango cha chini, matakwa yaliyoainishwa katika kanuni ya 37, kama ifuatavyo:	
	(a) jina kamili;	
	(a) tarehe ya kuzaliwa au tarehe ya usajili;	
	(b) jinsia;	
	(c) nambari ya kitambulishi cha muombaji ambacho kinaweza kuwa Kitambulisho cha Mzanzibar, Kitambulisho cha Taifa au Paspoti;	
	(d) eneo la makazi au sehemu ya biashara;	
	(e) kazi au aina ya biashara;	
	(f) madhumuni ya mkopo;	
	(g) sekta ya uchumi;	
	(h) kiasi cha mkopo kilichoombwa;	
	(i) dhamana itakayotolewa;	
	(j) hali ya ndoa;	

Na.	Jina la Nyaraka	Nyaraka Imeambatanishwa
	Mwombaji anatakiwa kuweka jibu (Ndio, Hapana, Haihusiki)	
	(k) idadi ya wategemezi;	
	(l) mwajiri	
	(m)kipato cha mwezi;	
	(n) kipato cha mwezi;	
	(o) matumizi ya mwezi;	
	(p) mikopo mingine inayodaiwa na wakopeshaji wengine; na	
	(q) taarifa nyengine yoyote zitakazohitajika na Benki.	
	Fomu ya maombi ya mkopo ioneshe sharti linalomtaka mwombaji kutoa idhini na tamko litakalowezesha kupata, kubadilishana au kuweka wazi taarifa zote za mikopo kulingana na masharti ya Sheria na Kanuni, kama inavyoelekezwa kwenye kanuni ya 35.	
8.	Mkataba wa mkopo uoneshe kwa kiwango cha chini, matakwa yaliyoainishwa katika Kanuni ya 38(2), kama ifuatavyo:	
	(a) kiasi cha mkopo;	
	(b) Madhumuni ya mkopo;	
	(c) Taarifa za dhamana ya mkopo;	
	(d) kiwango cha riba kwa awamu;	
	(e) kiwango cha riba kwa mwaka;	
	(f) ada na tozo nyengine zote;	
	(g) jadweli la marejesho ya mkopo linalojumuisha idadi ya marejesho, jumla ya kiasi cha kila rejesho kinachoonesha mkopo halisi, riba na ada tofauti, na tarehe ya kila rejesho;	
	(h) jumla ya malipo yote mpaka mkopo wote utakapokuwa umelipwa;	
	(i) njia ya kukokotoa kiwango cha riba;	
	(j) adhabu ya ucheleweshaji malipo na utaratibu wa ukokotowaji wake;	
	(k) ada, tozo au gharama za kukusanya mkopo ;.	
	(l) notisi ya kuonesha maslahi katika dhamana iliyotumika kudhamini mkopo;	
	(m)masharti ya ulipaji wa mapema wa mkopo;	
	(n) haki na wajibu wa mkopaji ikijumuisha masharti ambayo yatapelekea usitishwaji wa mkataba;	
	(o) haki na wajibu wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha; na	
	(p) majina na saini ya mkopaji na mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha.	
9.	Tamko la chanzo cha Mtaji na kwamba fedha hizo hazikupatikana kwa njia za uhalifu au kuhusishwa na shughuli yoyote ya uhalifu. (Tamko hilo ni lazima liwe limethibitishwa na Kamishna wa Viapo) kama ilivyoainishwa chini ya jadweli la tatu.	
10.	Uthibitisho wa uraia wa kila mwanahisa, mmiliki, mkurugenzi na afisa mtendaji mkuu aliyependekezwa. Hii inajumuisha picha mbili ndogo za hivi karibuni na mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo; (i) Nakala ya hati ya kusafiria (passport) iliyothibitishwa; (ii) Kitambulisho cha Taifa; au	

Na.	Jina la Nyaraka	Nyaraka Imeambatanishwa
	Mwombaji anatakiwa kuweka jibu (Ndio, Hapana, Haihusiki)	
	(iii) Kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi.	
11.	Dodoso lililojazwa kikamilifu na kila mmiliki, mjumbe wa bodi ya Usimamizi na afisa mtendaji mkuu kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha kama ilivyoelezwa katika Jadweli la tatu.	
12.	Taarifa za Mtu wa kuwasiliana naye zinazoonesha Jina lake, Anuani ya Posta, Namba ya Simu na Barua pepe (Taarifa hii ni lazima iwe ya mmiliki, mwanahisa au mjumbe wa Bodi ya kampuni)	
	B. Kwa taasisi	
	Pamoja na nyaraka zilizoorodheshwa katika kipengele **A** hapo juu, taasisi itawasilisha nyaraka zifuatazo:	
1.	Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili wa kampuni iliyothibitishwa na Uhakiki wa Usajili wa Kampuni kupitia BPRA.	
2.	Azimio la bodi ya Usimamizi linaloidhinisha Maombi ya leseni.	
3.	Taarifa za Mikopo za hivi karibuni kwa kila mmiliki, mjumbe wa bodi ya Usimamizi na afisa mtendaji mkuu .	
4.	Nakala ya taarifa za fedha iliyokaguliwa hivi karibuni kwa taasisi inayofanya kazi.	
	C: Kwa wakopeshaji binafsi	
	Pamoja na nyaraka zilizoorodheshwa katika kipengele A hapo juu, mkopeshaji binafsi atawasilisha nyaraka zifuatazo:	
1.	Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha jina la biashara.	
2.	Taarifa za Mikopo za hivi karibuni kwa kila mmiliki, mjumbe wa bodi ya Usimamizi na afisa mtendaji mkuu.	

Tamko la Mwombaji

Mimi, ……., ninakiri kwamba nimeambatisha nyaraka zote kama ilivyo ainishwa hapo juu kwa ajili ya maombi ya leseni ya mtoa huduma ndogo za fedha daraja la pili, na natambua kwamba maombi yasiyo na nyaraka zilizokamilika hayatapokelewa na Benki Kuu ya Tanzania.

…….. ……

Sahihi ya Mwombaji au Afisa aliyeidhinishwa **Tarehe**